**HOTUBA YA MHE. INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB), WAZIRI WA UJENZI KATIKA HAFLA YA UFUNGUZI WA JENGO MOJA (1) LA GHOROFA SABA (7) KWA AJILI YA MAKAZI YA WATUMISHI WA UMMA KATIKA ENEO LA MAGOMENI KOTA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM TAREHE 25 JUNI, 2024.**

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam;

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni;

Balozi Mhandisi Aisha S. Amour, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi,

Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo hapa;

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni;

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu;

Waheshimiwa Wabunge;

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Majengo Tanzania;

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania;

Waheshimiwa Madiwani;

Wenyeviti wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi,

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama Mbalimbali vya Siasa;

Waheshimiwa Viongozi wa Dini mliopo;

Watendaji Wakuu kutoka Taasisi mbalimbali;

Wafanyakazi wa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Majengo Tanzania;

Waandishi wa Habari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Ndugu Wageni Waalikwa,**

Awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutupatia afya njema na nguvu ya kuweza kukutana hapa leo.

Aidha, nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) Arch. Daud W. Kondoro kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika Hafla hii.

**Ndugu Wageni Waalikwa,**

Mbali na majukumu mengi ya Kitaifa niliyonayo, nimeona ni vyema nikashiriki pamoja nanyi katika jambo hili muhimu kwa watumishi wa Umma. Serikali inatambua umuhimu wa makazi bora kwa Wananchi wake ambapo mahitaji ya nyumba bora yanakadiriwa kuwa zaidi ya nyumba Milioni Tatu (3,000,000) Nchi nzima na yanaongezeka kwa kiwango cha takriban nyumba laki tatu na tisini (390,000) kila mwaka.

Aidha, nimefurahishwa sana na ubunifu na ujenzi wa nyumba za maghorofa unaofanywa na TBA. Hatua hii ya ujenzi wa nyumba za maghorofa katika miradi kama hii ni utekelezaji wa Sera ya Matumizi Bora ya Ardhi ya kujenga nyumba za kutosha kwa watumishi wa Umma.

**Ndugu Wageni Waalikwa,**

Mtendaji Mkuu wa TBA katika taarifa yake ameelezea historia ya uanzishwaji na uendelezaji wa maeneo kama haya ya Magomeni Kota na maeneo mengine ya Kota yaliyoko nchi nzima. Ninawakumbusha TBA kuendelea na Programu hii Maalum ya kuendeleleza maeneo yote yaliyorejeshwa Serikali Kuu kutoka TAMISEMI nchi nzima ili kuendana na ILANI ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-25, Ibara ya 55(h)(ii). Aidha, Wizara ya Ujenzi itaendelea kuhakikisha kuwa nyumba

hizi zinajengwa katika ubora unaostahili kwa gharama nafuu. TBA inatakiwa iangalie namna bora ya kupata wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuendeleza makazi kwenye maeneo kama haya ambayo yapo nchi nzima ili kutatua kero ya upungufu wa makazi kwa Watumishi wa Umma. Kufuatia Serikali kuruhusu Taasisi na Mashirika ya Umma kuingia ubia na Sekta Binafsi kama ambavyo Mtendaji Mkuu ameeleza, hii itarahisisha upatikanaji wa wabia na kuipatia Serikali nafasi kwa wataalam wake kujifunza teknolojia mpya kutoka kwa wabia wenza.

Nitumie fursa hii kuwaelekeza TBA kuharakisha ukamilishwaji wa miongozo kwa ajili ya ushirikishaji wa sekta binafsi na Taasisi za fedha kwa ajili ya uendelezaji wa milki ili kuwahudumia watumishi wa Umma wenye uhitaji wa makazi. Wizara ipo tayari kuwapatia ushirikiano wowote utakaohitajika. Hatua hii itaisaidia TBA kuondokana na utegemezi wa bajeti ya Serikali na hatimaye kujitegemea.

**Ndugu Wageni Waalikwa,**

Kama ilivyoelezwa na Mtendaji Mkuu wa TBA, Serikali imetoa fedha kiasi cha **Shilingi 5,686,583,190.00** (*Bilioni tano milioni mia sita themanini na sita laki tano themanini na tatu na mia moja tisini tu*) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma eneo la Magomeni Kota awamu ya pili 'B' hadi kukamilika kwake. Hivyo, ninapenda kuchukua fursa hii kuwataka Watumishi wa Umma ambao watapata fursa ya kupanga katika nyumba hizi, kuzitunza ili zibaki katika ubora wake, na kuzingatia masharti ya mkataba wa upangaji ikiwemo **kulipa kodi kwa wakati.** Ninapenda kutoa pongezi kwa TBA kwa kubuni mbinu za kisasa za kuhakikisha wapangaji hawalimbikizi madeni ya kodi ya pango kwa kuweka mfumo unaomfanya mpangaji kushindwa kupata

huduma ya umeme kama hajalipa kodi. Hongera sana Mtendaji Mkuu na timu yako ya wataalam. Nitumie pia fursa hii kusisitiza maelekezo yangu ambayo nilishayatoa kuhusu zoezi la kudai madeni kwa wadaiwa sugu na kuwatoa kwenye nyumba liwe endelevu bila kubagua.

**Ndugu Wageni Waalikwa,**

Kwa namna ya kipekee ninapenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuiamini Wizara ya Ujenzi inayotekeleza miradi ya Ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali kupitia TBA, kwa kutoa fedha zinazowezesha utekelezaji wa Miradi mbalimbali ukiwemo mradi huu niliouzindua leo.

**Ndugu Wageni Waalikwa,**

Baada ya kueleza haya, ninawataarifu kuwa jengo la makazi ya watumishi wa umma la Magomeni Kota awamu ya pili B limekwishafunguliwa rasmi.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**